

## MIAKA 2 YA RAIS SAMIA

# Mifugo inavyochochea ukuaji uchumi



Sekta ya mifugo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na pato la taifa.. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MIFUGO ni moja ya sekta muhimu ambazo ni tegemeo kwa maendeleo ya uchumi nchini. Kutokana na umuhimu huo, serikali imekuwa ikiweka vipaumbele mbalimbali katika kuendeleza sekta hiyo ikiwamo kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika ufugaji ukiwamo wa kibiashara.

Sambamba na hilo, serikali pia imekuwa ikivutia uwekezaji wa viwanda vya mazao ya mifugo kama vile nyama, ngozi na maziwa ili kuleta tija na maendeleo ya kiuchumi kupitia sekta hiyo. Kadhalika msisitizo umekuwa katika ubora wa mazao ya mifugo ili kupata masoko ndani na nje ya nchi pamoja na ushindani dhidi ya kampuni zingine za nje zinazozalisha bidhaa hizo.

Tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani takriban miaka miwili iliyopita, ameweka mkazo mkubwa katika sekta ya mifugo kwa dhamira ya kuhakikisha inachangia kikamilifu katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Tanzania inakadiriwa kuwa nchi ya tisa duniani na ya tatu Afrika kuwa na idadi kubwa ya ng'ombe.

Aidha, kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania ina ng'ombe milioni 35.3, mbuzi milioni 25.6, kondoo milioni 8.5, kuku milioni 93 (wakiwamo wa kisasa milioni 50.3 na wa kienyeji milioni 42.7) na nguruwe milioni 3.4 kwa takwimu hizo, ni dhahiri kwamba sekta ya mifugo ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya uchumi pamoja na kubadilisha hali za maisha ya Watanzania walio wengi kiuchumi na kijamii.

### DHAMIRA YA RAIS

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia, yako mambo mengi ambayo yamefanyika katika kuhakikisha mifugo inatoa mchango unaostahili kwa maendeleo ya uchumi, ikiwamo mageuzi katika sekta ya viwanda.

Kutokana na umuhimu huo, akifungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo jijini Dodoma Desemba, 2022 uliokuwa na kaulimbiu: "Mwelekeo Mpya wa Sekta ya Mifugo Tanzania", Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alisema Rais Samia ana mapenzi ya dhati na sekta hiyo na kiu yake ni kuona inaleta mapinduzi ya kiuchumi.

Majaliwa alisema Rais Samia anatamani kuona mifugo inakuza zaidi pato la wananchi, kutoa ajira na kuchangia pato la taifa bila kuathiri mazingira na maendeleo ya sekta zingine.

Pamoja na kiu hiyo, Rais Samia ameonyesha kwa vitendo, ameongeza fedha katika bajeti ya serikali ya mwaka 2022/23 kwa ajili ya maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kutoka Sh. bilioni 121.3 (mwaka 2021/22) hadi Sh. bilioni 168.24.

Pia katika kuboresha huduma za mifugo na kuiepusha dhidi ya magonjwa, Rais Samia ametoa Sh. bilioni 5.9 kwa ajili ya ujenzi wa majosho 257 katika halmashauri 80 na tayari majosho 88 yamekamilika. Licha ya ujenzi wa majosho hayo, serikali katika kipindi cha miaka miwili imetoa dawa ya ruzuku kwa ajili ya kuweka kwenye majosho lita 52,560 nchini kote zenye thamani ya Sh. bilioni 2.3.

### MAZAO YA MIFUGO

Ili kuhakikisha mifugo inachangia ipasavyo pato la taifa, kuna mambo mbalimbali yaliyofanyika na yanaendelea kufanyika ikiwamo upatikanaji wa mazoa bora ya mifugo yenye uwezo wa kukidhi soko la ndani na la nje. Mazao kama nyama, maziwa na ngozi vinavyozalishwa nchini, vinatakiwa kuwa na viwango na ubora wa kimataifa ili kuleta ushindani katika soko la dunia.

Ubora ni jambo la msingi katika sekta yoyote na katika kufanikisha hilo, serikali imedhamiria kuwa na mifugo bora kwa kufanya utafiti wa mbegu bora kwa ajili ya uzalishaji mifugo bora.

Pia serikali imejenga majosho katika maeneo

INAENDELEA UKURASA VII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA (BUWASA)

**Salamu za Pongezi**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA) wanaungana na Watanzania kukupongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wako.

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wako, tumeona maboresho na mabadiliko makubwa katika sekta ya maji na sisi kama BUWASA tumeguswa na mabadiliko hayo na hivyo tunakupongeza kwa jitihada mbalimbali unazochukua ikiwamo kuongeza bajeti katika sekta ya maji.

BUWASA tunaahidi kuendelea kuunga mkono kwa dhati serikali ya awamu ya sita kwa kuhakikisha tunatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya kumtua mwanamke ndoo kichwani kwa kufanya kazi kwa bidii na kuzidi kuleta maendeleo katika sekta ya maji nchini.



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

*Kazi Iendelee*

*Maji ni Uhai Tutunze Miundombinu ya Maji kwa Pamoja*

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA - BUWASA
S.L.P 81, BUKOBA, Baruapepe : info@buwasa.go.tz
Tovuti : www.buwasa.go.tz
TUPIGIE SIMU BURE: 0800 712080 AU 0800 110146
BUWASA



# Mifugo inavyochochea ukuaji uchumi

INATOKA UKURASA VI

mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha afya ya mifugo inaimarika sambamba na kusambaza chanjo kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo.

Kwa upande wa uzalishaji bora wa ngozi, serikali imeboresha machinjio na kuimarisha viwanda vya ngozi katika mikoa ya Morogoro, Kagera, Geita na Kilimanjaro ambayo yamewezesha pia upatikanaji wa ngozi zenye ubora wa kimataifa kwa asilimia 80 hadi 85.

Aidha, mauzo ya nyama katika soko la nje umeongezeka. Kwa mwaka 2021/22 zaidi ya tani 10,000 za ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na kondoo ziliouzwa nje na kuingiza dola za Kimarekani milioni 36.2.

Pamoja na biashara ya nyama ndani na nje ya nchi, uzalishaji wa maziwa pia umeongezeka kutokana na uwapo wa zaidi ya viwanda 110 katika maeneo mbalimbali nchini.

Ili kupanua wigo zaidi wa mauzo ya nyama nje ya nchi, serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, imeanzisha juhudi za kufungua masoko



Serikali ya awamu ya sita imekuwa ikivutia wawekezaji katika viwanda vya kusindika nyama kwa soko la ndani na la nje.

Hong Kong, Vietnam, Kuwait, Falme za Kiarabu (UAE), Oman, Jordan, Bahrain na Comoro.

Licha ya kufungua masoko hayo, serikali ya awamu ya sita imeanzisha mpango kabambe wa kuwavutia wawekezaji kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi.

Katika kuhakikisha sekta hiyo inachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi, serikali pia imedhamiria kupanua wigo wa udahili wa wanafunzi katika vyuo vikuu na vya kati kikiwamo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kutoa wataalamu wa kada mbalimbali wa mifugo. Mbali na SUA, udahili unaongezwa zaidi katika kampasi nane za Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA).

Kupatikana kwa wataakamu hao kutawezesha kuwapo kwa mifugo bora yanye afya kwa kuwa shughuli za utafiti na ugani zitaimarishwa na kuboreshwa. Hatua hiyo itawawezesha wWananchi waliokuwa wakifuga kwa njia zisizo za kitaalamu, kupata uwezo wa kuendesha shughuli zao kwa utaalamu kutokana na kuwapo maofisa mifugo na ugani.

CamScanner

uongozi wa kampuni hiyo ulipinga na kusema kuwa

hiwa na ofisi yake kama kweli yanatoka kitalu B au C.

HABARI LEO UK 5.

# Majosho 6 ya Sh mil 108 yakamilika Njombe

**Na James Kasanga, Njombe**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekamilisha ujenzi wa majosho sita ya kuogeshea mifugo yenye thamani ya Sh 108,000,000 katika Halimashauri ya Mji Njombe.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Mbunge wa Jimbo la Njombe mjini, Deo Mwanyika alisema majosho yaliyojengwa ni pamoja na josho la Makowo, Mikongo, Iwungilo, Ngalanga, Lilombwi na Igaba.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha inasogeza huduma kwa wafugaji na hivyo kuwataka waongeze kasi ya ufugaji.

Aidha aliwataka wafugaji kutumia fursa ya uwepo wa majosho hayo kwa kuhakikisha mifugo inaogeshwa.

CamScanner




# Mafanikio sekta ya uvuvi

Na Magnus Mahenge

SEKTA ya uvuvi ni moja ya sekta za kiuchumi inayochangia katika lishe, kipato, fedha za kigeni na kukuza uchumi kwa ujumla. Sekta inajumuisha tasnia za uvuvi katika maji ya asili na ukuzaji viumbe maji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega katika taarifa yake ya miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan, anasema mafanikio mengi yamepatikana katika sekta ya uvuvi.

UVUVI

Serikali imeingia mkataba na wazabuni wawili kwa ajili ya kutengeneza na kusambaza boti za kisasa za fibre za thamani ya Sh bilioni 11.5 zitakazotolewa kama mkopo wa masharti nafuu usio na riba kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Wananchi 2,753 wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi wanatarajiwa kunufaika.

Kuanza kwa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko, Lindi ambapo tayari Mkandarasi China Harbour Engineering Company Ltd amepatikana na ujenzi ulianza rasmi Septemba, 2022 na unatarajiwa kukamilika 2024.

Bandari hii muhimu kitaifa ni kielelezo inatazamiwa kuigharimu serikali Sh bilioni 280. Bandari itapokea meli tatu hadi 10 kwa wakati mmoja na boti 30 za wavuvi wadogo kwa wakati mmoja.

Wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokelea samaki ya Kayenze (Ilemela), New Igombe (Ilemela) na Ihale (Busega). Aidha, ujenzi na ukarabati wa mialo ya Chifunfu (Sengerema) na Igabiro (Bukoba) unaendelea.

Pia ujenzi wa Soko la Samaki la Mbamba Bay (Nyasa) umekamilika. Ujenzi na ukarabati umeigharimu serikali Sh milioni 708.5.

Kuwezesha ujenzi majengo matano ya ofisi za vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMU) za thamani ya Sh milioni 778.4 katika Wilaya za Pangani (Kipumbwi), Mkinga (Zingibari), Lindi Vijijini (Sudi), Bagamoyo (Dunda) na Chalinze (Saadani) kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Pwani.

Serikali imenunua boti za doria 16 na injini za kupachika 17 vya thamani ya Sh milioni 463.4 na ambazo zimepelekwa katika vituo na vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

Pia imeimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya uvuvi ambapo juhudi za serikali zimefanikisha kufunguliwa kwa soko la mazao ya uvuvi hususani mabondo katika Jamhuri ya Watu wa China ambayo yalikuwa awali hayauzwi moja kwa moja nchini humo.

Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) limefufuliwa ambapo Mtendaji Mkuu amepatikana na Bodi imeundwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa majukumu yakiwemo ununuzi wa meli; ujenzi wa viwanda na miundombinu ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na kuendesha shirika kibiashara.

Kutungwa kwa sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 pamoja na kuandaa kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2021 ambayo imeleta vitutio na kuwezesha kukatwa leseni 69 za meli za uvuvi.

Leseni hizo zimekuwa chanzo cha kuingiza Pato la Taifa ambapo katika fedha hizo asilimia 50 inagawanywa kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) kwa kupata asilimia 30 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa kupata asilimia 20 na asilimia 50 ni kwa ajili ya kuendesha mamlaka.

Serikali katika kuhakikisha rasilimali za uvuvi za bahari kuu zinanufaisha taifa, Mamlaka imeingia makubaliano ya uvuvi na Kampuni ya ALBACORA Group kutoka Hispania ikiwa ni juhudi za kuvutia uwekezaji wa bahari kuu.

Aidha, pamoja na kulipia leseni ya uvuvi ya kiasi cha Dola za Marekani 21,000, pia kampuni imelipa kiasi cha Dola za Marekani 400,000. Vilevile imeshusha nchini kiasi cha tani 100 za samaki kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki.

Kwa mara ya kwanza katika kipindi cha takribani miaka 30, serikali imefanikiwa kufanya utafiti wa uwingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa ziwa hilo upande wa Tanzania, kuna kiasi cha tani 144,690 za samaki.

Matokeo ya utafiti yatawezesha serikali kuweka mipango madhubuti ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi jamii ya dagaa na migebuka Ziwa Tanganyika.

Serikali kupitia Tafiri kwa kutumia setelaiti inawasaidia wavuvi wadogo kubaini maeneo yenye samaki kwa wingi katika Bahari ya Hindi ili kuwapunguzia gharama za uvuvi na muda wa uvuvi.

UKUZAJI VIUMBE MAJI

Wazari Ulega anasema kumekuwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya viumbe maji kutoka tani 22,793.20 hadi kufikia tani 28,856.87 za thamani ya Sh bilioni 184.7.

Kuongezeka uwekezaji wa ufugaji samaki kibiashara kutoka Sh bilioni 11 hadi bilioni 17. Sehemu kubwa ya uwekezaji kwa njia ya vizimba kutoka vizimba 473 hadi 780 vya kuweza kuzalisha takribani tani 5,000 kwa mwaka.

Kuongezeka kwa uzalishaji wa vifaranga vya samaki na kambamiti kutoka milioni 24.2 hadi milioni 31.4. Pia matumizi ya chakula chenye ubora yaliongezeka kutoka tani 1,182.47 hadi 2,156.1.

Kuongezeka kwa idadi ya vifaranga vinavyopandikizwa katika malambo kwa mwaka ili kuongeza upatikanaji wa samaki kutoka 101,500 hadi 373,200.

Kubainisha maeneo 28 yanayofaa kwa ufugaji samaki kwa vizimba kwenye Ziwa Victoria katika mikoa ya Mwanza na Kagera na kuyafanyia tathmini ya kimkakati ya mazingira ili kuwapunguzia gharama za uwekezaji kwa wafugaji samaki.

Kuingia mkataba na wazabuni sita kwa ajili ya kusambaza pembejeo na zana za thamani ya Sh bilioni 17.85 zitakazotolewa kama mikopo ya masharti nafuu isiyo na riba kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Jumla ya wafugaji samaki 3,154 na wakulima wa mwani 2,030 wanatarajiwa kunufaika.

Aidha, kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba kwa ajili ya wafugaji wa samaki kwa kutumia teknolojia ya vizimba. Mradi huu unatarajiwa kuchangia katika kufikia lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki wa kufugwa kwa mwaka kutoka tani 25,000 hadi tani 50,000 na mwani kutoka 3,500 hadi tani 10,000 ifikapo 2025/2026.

Kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa mashamba darasa sita ya ufugaji samaki ya thamani ya Sh milioni 741.9 katika halmashauri sita za Kongwa, Iringa, Njombe, Songea, Tandahimba na Ruangwa.

Lengo la mashamba darasa haya ni kusogeza huduma za ugani kwa wananchi kuongeza mwamko wa ufugaji samaki. Awamu ya pili itajumuisha ujenzi wa mashamba darasa manane yenye thamani ya Sh bilioni 1.058 katika halmashauri za Dodoma Jiji, Iramba, Uyui, Maswa, Bariadi, Moshi, Mwanga na Mkuranga.

Jumla ya wananchi 12,902 wamepatiwa mafunzo mbinu bora za ufugaji samaki, udhibiti wa magonjwa ya samaki pamoja na uzalishaji na uhifadhi wa zao la mwani.

Vilevile, maofisa ugani 59 kutoka katika ngazi ya halmashauri wamepatiwa mafunzo rejea kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki kuwaongezea ufanisi katika kutoa huduma za ugani.

